

KAJA NIZURU

1. Hoye! Hoye! Shangilizi, kutoka kwangu moyoni,
Hoye! Hoye! Za mbawazi, ziningile haibani,
Hoye! Hoywe! Maliwazi, sababu nawayuzani,
Kaja nizuru nyumbani, nduya' Hassan Adamu.
2. Nduya Hassani Adamu, kaja nizuru nyumbani,
Ugeni wake muhimu, ulingiya dosarini,
Hatukulaliza hamu, kawa kiguu ndiyani,
Kulekea Jarumani, nduya' Hassani Adamu.
3. Alikitokeya Tanga, achenenda Jarumani,
Kwa mahaba kajifunga, kapija hodi langoni,
Kunizuru Andanenga, hapa Shamba Kinondoni,
Kwa yake kubwa hisani, nduya Hassani Adamu.
4. Ilikuwa asubuhi, hamuuzi ndiwe nani?
Akiwa amefurahi, kanamba ndimi Hassani,
Akaniaga "nawahi", kwenye ndege kiwanjani,
Hatukulonga kwa ndani, nduya Hassani Adamu.
5. Kwa huo muda mchache, nawapani ya yakini,
Na kwa nini niwafiche, tabia yake mwendani,
Kanaifanya aniwache, asitoke kumbukoni,
Kwa njema yake lisani, nduya Hassani Adamu.
6. Hampa kisa halisi, chui kugeuka nyani,
Simba kugeuka fisi, chuma kugeuka kuni,
Jiti kugeuka nyasi, niwajuzao shikeni,
Kamakinika makini, nduya Hassani Adamu.
7. Tamati naihandisi, kwa matama na huzuni,
Mwana wa nyoka mjusi, haogopwi abadani,
Hatunao wasiwasi, si mwenye sumu kanwani,
"JUA" lisihatiani, nduya Hassani Adamu.

Amiri A.S. Andanenga (Sauti ya Kiza)
Kinondoni, Shamba
DAR ES SALAAM, Tanzania.